Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Mei

TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.06 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz

HALIUZWI

Bima ni Kinga, Bima ni Ngao, Bima ni Maendeleo

Yaliyomo

01

03

Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma

Mhariri
Hadija Maulid

Waandishi
Tabia Mchakama
Anna Massao

Msanifu
Abubakari W. Kafumba

TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRAUpdates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Mei 2025.

01 Udanganyifu katika Bima Sio tu ni Kosa la Jinai – Ni Kikwazo cha Maendeleo - Mhe. Mkuya

03 Dkt. Saqware Awapongeza Suma JKT Kuanzisha Suma JKT Life Insurance

05 Naibu Kamishna wa Bima Azindua Rasmi Akiba Flex Plan: Suluhu Bunifu la Akiba na Ulinzi wa Maisha kwa Watanzania

07 Tunaboresha Taswira ya jengo: Ofisi za Makao Makuu TIRA Mbioni Kukamilika

09 Dkt Saqware: Vijana mna Nafasi Kubwa ya Kuleta Mabadiliko Sekta ya Bima Kupitia Ubunifu

11 Uelimishaji wa Bima kwa Njia ya Fasihi: Visa na Mikasa Kumi na Moja Vyaandikwa

13 Bima Debate Mtanange wa Kielimu Kukuza Uelewa wa Bima Nchini

12 Bima Sports ilivyokonga Nyoyo: Wadau Sekta ya Bima Waonesha Uwezo katika Kabumbu na Michezo Mingine

16 TIRA Yashiriki Tanzania Dental Expo: Karibu Ufahamu Wajibu Wetu kwa Watoa Huduma za Afya

17 TIRA yatoa Elimu ya Bima Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo

Scan
Kusoma Kidijiti

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
info@tira.go.tz

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
www.tira.go.tz

Udanganyifu katika Bima Sio tu ni Kosa la Jinai – Ni Kikwazo cha Maendeleo - Mhe. Mkuya

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Mhe. Saada Mkuya aliyasema hayo Mei 16, 2025 akiwa ni mgeni rasmi katika Uzinduzi wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Wataalamu wa Uchunguzi wa Udanganyifu katika masuala ya Bima (IASIU) uliofanyika ukumbi wa PAPU, jijini Arusha na kusisitiza juu ya uundwaji wa mikakati dhabiti kuzuia udanganyifu katika bima. Aidha, Mhe. Mkuya pia aliipongeza TIRA na Jumuiya ya wataalamu hao (IASIU – Tanzania) kwa kuandaa mkutano huo wenye tija katika sekta ya bima.

Awali, Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware katika hotuba yake alieleza mikakati iliyofanywa na Mamlaka na kusema "Kwa upande wetu kama Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), tumeweka mikakati madhubuti ili kukabiliana na changamoto hii. Tumeanzisha mifumo ya kisasa ya kudhibiti taarifa na kufuatilia madai ya bima kwa ukaribu zaidi".

Naye, Rais wa IASIU Tanzania Bw. Mjabwa Hanzuruni katika hotuba yake, alieleza Jumuiya hiyo ina lengo la kukuza uaminifu katika kugundua, kuchunguza na kuzuia udanganyifu katika bima kwa njia bora na za kisasa. Mkutano huo wa siku tatu ulifungwa rasmi Mei 16, 2025.

iasiu
IASIU LAUNCHING AND ANNUAL CONFERENCE
THEME
COLLABORATION & TECHNOLOGY:
TACKLING INSURANCE FRAUD TOGETHER
IASIU TANZANIA CHAPTER LAUNCHING AND ANNUAL CONFERENCE
COLLABORATION & TECHNOLOGY: TACKLING INSURANCE FRAUD TOGETHER
Britam
Allianz
Strategis
ARIS
iasiu

iasiu
iasiu

Dkt. Saqware Awapongeza Suma JKT Kuanzisha Suma JKT Life Insurance

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) Mei 10 2025, iliungana na wadau wengine katika sekta ya bima kushuhudia uzinduzi wa Kampuni ya Bima ya Maisha inayoitwa Suma JKT Life Insurance katika hafla fupi iliyofanyika katika Ukumbi wa The Super Dome Masaki jijini Dar es Salaam, ambapo Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware aliwapongeza kwa kuanzisha kampuni hiyo na kuwakaribisha rasmi katika sekta ya bima.
Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Jenerali Jacob J. Mkunda.

Lakini pia Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alishiriki na katika hotuba yake alitoa rai kwa kampuni hiyo kufanya kazi kwa weledi, uaminifu, uadilifu na kuwajali wateja lakini zaidi kuwa wabunifu na kuendana na kasi ya ukuaji wa sekta ambayo inakua kwa asilimia 5% na kuahidi ushirikiano kutoka Mamlaka katika kutekeleza majukumu yao.

Awali pia Bi. Flora Minja, Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni za Bima Tanzania (ATI) katika hotuba yake aliwaahidi ushirikiano na kuwapongeza kwa hatua hiyo muhimu katika sekta ya bima.

Uzinduzi huo ulihitimishwa rasmi na Mgeni Rasmi Jenerali Mkunda ambaye katika hotuba yake aliishukuru Mamlaka kwa ushirikiano walioonesha katika kufanikisha usajili wa kampuni hiyo na kuongeza nia ya Jeshi pia ni kuendelea kuchangia katika Uchumi wa nchi kuongeza pato la taifa kupitia Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa yani Suma JKT.



SUMAJKT®
LIFE INSURANCE

Naibu Kamishna wa Bima Azindua Rasmi Akiba Flex Plan: Suluhu Bunifu la Akiba na Ulinzi wa Maisha kwa Watanzania

Tarehe 20 Mei 2025, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ilishiriki katika uzinduzi rasmi wa bidhaa mpya ya Akiba Flex Plan kutoka kampuni ya Jubilee Life Insurance, bidhaa iliyobuniwa mahsusi kuwasaidia watanzania kuwekeza fedha zao huku wakijihakikishia ulinzi wa maisha yao. Hafla hiyo ya uzinduzi ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya bima, taasisi za kifedha, pamoja na wawakilishi kutoka serikalini.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Bima Tanzania, Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said, aliipongeza kampuni ya Jubilee Life Insurance kwa kuendelea kuonesha ubunifu unaolenga kutoa suluhu ya kweli kwa changamoto za kifedha zinazowakumba Watanzania wa makundi yote. Alisema kuwa bidhaa kama Akiba Flex Plan sio tu kwamba inatoa fursa ya kujiwekea akiba, bali pia inahakikisha kuwa wananchi wanapata ulinzi wa maisha yao kupitia bima, muunganiko wa kipekee wenye manufaa makubwa kwa mtu binafsi na familia yake.

Bi. Khadija alisisitiza kuwa upatikanaji wa bidhaa jumuishi kama Akiba Flex Plan ni hatua madhubuti ya

kuwawezesha wananchi kupanga maisha yao ya baadaye kwa usalama na uhakika. Aidha, alieleza kuwa Mamlaka itaendelea kusimamia upatikanaji wa huduma bora za bima kwa wote, huku ikisisitiza ulipaji wa madai kwa wakati ili kuongeza imani ya wananchi katika sekta hiyo muhimu ya uchumi.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Jubilee Life Insurance, Bw. Amyn Lalji, alisema kuwa Akiba Flex Plan ni jibu la kimkakati kwa mahitaji yanayobadilika ya wateja waliopo na wale wapya.

Alieleza kuwa bidhaa hiyo inaleta pamoja unafuu wa kifedha, nidhamu ya kuweka akiba, na urahisi wa matumizi ya kidijitali kwa pamoja. Alisema kuwa ili kukidhi kasi ya mabadiliko ya kiuchumi, ni muhimu kwa watoa huduma kama Jubilee kuendelea kubuni bidhaa bunifu zinazogusa mahitaji ya kweli ya jamii. Aliongeza kuwa anaamini Akiba Flex Plan itawawezesha Watanzania kufikia malengo yao ya kifedha wakiwa kinga ya bima.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life Insurance, Bi. Helena Mzena, alifafanua kuwa bidhaa hiyo inalenga kuziba pengo kati ya ulinzi wa kifedha na uhuru wa michango ya mteja. Alisema kuwa Akiba Flex Plan inaonesha dhamira ya Jubilee kuleta bima karibu zaidi na maisha ya Mtanzania wa kawaida.

"Bima si tu bidhaa ya kifedha, bali ni ahadi ya ulinzi, utu na amani ya moyo," alisema Bi. Helena, akiongeza kuwa bidhaa hiyo imetengenezwa mahusus kwa watu ambao hawajawahi kupata huduma rasmi za bima ya maisha, pamoja na wale ambao tayari wanatumia bima lakini wanahitaji chaguo la ziada lenye unafuu na ufanisi.

Uzinduzi huu unathibitisha kuwa sekta ya bima nchini Tanzania inaendelea kukua kwa kasi, huku bidhaa kama Akiba Flex Plan zikionesha njia mpya na bunifu za kuongeza ushiriki wa wananchi katika huduma rasmi za kifedha, kwa ajili ya ustawi wa mtu mmoja mmoja na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Tunaboresha Taswira ya jengo: Ofisi za Makao Makuu TIRA Mbioni Kukamilika

Jengo la Makao Makuu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), linalojengwa jijini Dodoma eneo la Njedengwa lipo katika hatua za mwisho kukamilika ambapo Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma – TIRA hapo Mei 5, 2025 kilitembelea jengo hilo.

Ziara hiyo ililenga kuhakikisha kuwa taswira ya TIRA inaakisi maono yake, majukumu na mikakati yake mbalimbali.

Azma ya TIRA ni kuhakikisha muonekano wa Ofisi hiyo unakuwa nadhifu na wenye kupendeza katika kuhudumia wadau mbalimbali.

Muonekano wa chapa madhubuti husaidia kutoa ujumbe unaoeleweka kwa haraka, kuimarisha utambulisho wa taasisi, na kuleta mvuto kwa wadau mbalimbali wakiwemo kampuni za bima, watumiaji wa huduma na washirika wa maendeleo.

Jengo hilo sio tu lina ofisi za kutosha kwa watumishi wake bali pia kumbi mbalimbali za mikutano na sehemu za kupumzika kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi ambao TIRA ina jukumu kubwa la kuhakikisha wanapata huduma stahiki kwa wakati na haraka.

SAMSUNG

Dkt Saqware: Vijana Mna Nafasi Kubwa ya Kuleta Mabadiliko Sekta ya Bima Kupitia Ubunifu

Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware aliyasema hayo wakati akitoa hotuba yake kwa wadau walioshiriki Bima Debate iliyofanyika jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa chuo cha ACISP Masaki tarehe 24 Mei 2025.

Dkt. Saqware alisisitiza umuhimu wa vijana; wanafunzi wa sekondari na wanavyuo wasomi wabobezi masuala ya bima kuangalia changamoto mbalimbali katika soko na kuwa wabunifu kutatua.

Dkt. Saqware pia alisisitiza Mamlaka imechukua hatua mbalimbali kukuza ukuaji wa soko la bima nchini ambapo kwa miaka mitano (5) mfululizo soko linakua kwa asilimia 15% kila mwaka hii ikiangazia viashiria mbalimbali kama ongezeko la watoa huduma wa bima, ongezeko la ajira katika sekta, ubakizwaji wa ada ya bima nchini na mambo mengine mbalimbali.

Kamishna pia alizipongeza shule na vyuo vilivyoshiriki, majaji na waandaaji wa Bima Debate kufanikisha tukio hilo muhimu katika kukuza uelewa wa bima nchini. Bima Debate hiyo ilifanyika kama shamrashamra za kuelekea Siku ya Bima kitaifa Tanzania (Tanzania Insurance Day 2025) na iliandaliwa na Taasisi ya Bima Tanzania (IIT) kwa kushirikiana na TIRA.

BIMA
DEBATE

BIMA
DEBATE

Uelimishaji wa Bima kwa Njia ya Fasihi: Visa na Mikasa Kumi na Moja Vyaandikwa



Mei 28, 2025 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilishuhudia uzinduzi wa vitabu kumi na moja (11) vyenye hadithi za kusisimua kuhusu umuhimu, mafanikio na mafunzo ya bima kwa jamii. Tukio hilo liliandaliwa na Tanzania Fasihi Fund (TAFF) na lilifanyika katika viwanja vya Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam.

Vitabu hivyo vimeandikwa na waandishi mahiri kutoka Tanzania na nchi jirani. Baadhi ya majina ya vitabu hivyo ni pamoja na Hazina, Fanikio Aridhini, Kibaruani, Kiburi si Muungwana, Najutia nafasi, Joto na Jasho baharini, Bima Mujarabu, Hazina ya Ukaidi na vingine mbalimbali.

Akitoa neno la Shukrani katika Tamasha hilo la tatu la Fasihi Mkurugenzi wa TAFF, Bw. Hussein Wamaiya aliishukuru TIRA kwa kuonyesha njia katika kuunga mkono kazi za sanaa na kuzitumia kama njia ya kuelimisha jamii kuhusu bima. Lakini pia kuwa mdhamini mkubwa katika tamasha hilo.

Aidha, kwa upande wa Mamlaka iliwakilishwa na Meneja wa Uhusiano na Mawasiliano, Bi. Hadija Maulid kwa niaba ya Kamishna wa Bima aliushukuru uongozi wa TAFF kwa heshima waliyoipa TIRA na sekta ya bima kwa ujumla na kusisitiza lengo la sekta ya bima ni kufikia azma ya Serikali kuwa ifikapo mwaka 2030 kupata asilimia 80 ya watanzania wenye uelewa kuhusu bima na asilimia 50 ya wanaotumia bima hivyo njia mbalimbali za kuelimisha zinatumika kufikia lengo hilo.

BAKIZA
FANANI MPOLE
PRINTERS
UWAVITA

BAKITA
FANANI MPOLE
MACS
Community Empowerment

Bima Debate Mtanange wa Kielimu Kukuza Uelewa wa Bima Nchini

Tarehe 24 Mei 2025, Bima Debate ilifanyika katika ukumbi wa chuo cha ACISP ambapo shule mbalimbali za Sekondari kutoka mkoa wa Dar es Salaam zilikutana kujadiliana na kutoa maoni kuhusu mada mbalimbali, ikiwemo inayosema Je Bima inasaidia kukuza uchumi wa Tanzania? Lakini pia mada inayohusu umuhimu wa bima ya afya kwa jamii.

Mgeni Rasmi alikuwa Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware.

Aidha, Bima Debate hiyo ilifanyika kama sehemu ya kionjo kuelekea Siku ya Kitaifa ya Bima Tanzania (Tanzania Insurance Day) itakayofanyika June 18 -21 jijini Arusha na iliandaliwa na Taasisi ya Bima Tanzania (IIT) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

Shule zilizoshiriki Bima Debate hiyo ni pamoja na Shule ya Sekondari Jangwani, Zanaki, Midland, Shaaban Robert na Kisutu Sekondari.

Bima Debate hiyo ilikuwa sehemu ya mikakati ya sekta ya bima katika kukuza uelewa wa masuala ya bima nchini ambapo pia ni muhimu kuanzia kwa watoto na vijana ambao ni taifa la kesho.

BIMA
DEBATE


BIMA
DEBATE

BIMA


BIMA
DEBATE
SCHEDULE
JUDGE
JUDGE
JUDGE

Bima Sports ilivyokonga Nyoyo: Wadau Sekta ya Bima Waonesha Uwezo katika Kabumbu na Michezo Mingine

Mei 31, 2025 ilikuwa siku njema sana kwa wapenzi wa michezo hasa wadau sekta ya bima, Bima Sports ilipamba moto katika viwanja vya Tanzanite Sports Hub Mikocheni.

Katika tukio la kusisimua zaidi Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware alichezesha mechi ya mpira wa miguu (football) iliyowakutanisha wakuu wa kampuni za bima.

Michezo ni afya, Bima Sports ni kionjo kingine katika shamrashamra za kuelekea Siku ya kilele cha Bima Tanzania ambapo kwa mwaka huu wa 2025 tukio hilo litafanyika June 18 – 21 jijini Arusha.

Bima Sports ilikuwa na michezo mbalimbali ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu, riadha na mchezo wa kukimbiza kuku.

Timu ya mpira wa miguu kutoka Mamlaka ilishiriki na kufanya vizuri lakini bahati ya mtende kwa mwaka huu iliwaangukia kampuni ya Bima ya CRDB ambao walitwaa kombe.

Aidha, ushindi mwingine ulienda kwa raisi wa taasisi ya bima (IIT) Bi. Margaret Ikongo aliyeibuka kidedea katika mchezo wa kukimbiza kuku.

TIRA Yashiriki Tanzania Dental Expo: Karibu Ufahamu Wajibu Wetu kwa Watoa Huduma za Afya

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kupitia Kanda ya Mashariki ilishiriki maonesho ya siku mbili ya 'Tanzania Dental Expo" ambayo yalikusanya watoa huduma za kinywa na meno, pamoja na wadau wengine wa afya. Maonesho hayo yalifanyika mlimani city, Dar es salaam na yalianza Mei 30 – 31 2025.

Aidha, katika maonesho hayo TIRA ilitoa elimu ya bima kwa washiriki lakini pia watoa huduma za afya walipewa rai ya kufanya usajili kupitia mfumo wa ORS. TIRA ina jukumu la kusajili vituo vya afya vinavyotoa huduma kupitia bima za afya.

Maonesho hayo yalikuwa ni muendelezo wa utoaji elimu ya bima kwa umma ili kuweza kufikia malengo ya Mamlaka na ya Serikali kwa ujumla kuongeza uelewa na matumizi ya bima nchini.

TIRA yatoa Elimu ya Bima Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kanda ya kati, Dodoma ilitoa elimu ya bima kwa wanachuo wa Chuo cha Serikali za Mitaa kilichopo Hombolo Mei 20, 2025 jijini Dodoma. Elimu hiyo ililenga kuwawezesha wanafunzi kuelewa dhana ya bima, aina mbalimbali za bima, umuhimu wa kuwa na bima, pamoja na majukumu ya TIRA katika kusimamia sekta ya bima nchini.

Aidha, wanachuo hao walipata fursa ya kuuliza maswali na kushiriki katika majadiliano kuhusu mafanikio na changamoto wanazoziona katika masuala ya bima na pia kueleza namna watakavyoweza kusambaza elimu hiyo kwa watu hao wa karibu ii waweze kutumia huduma za bima kujikinga na majanga mbalimbali.

Zaidi kupitia elimu hii, TIRA inaendelea kutekeleza jukumu lake la kuelimisha umma kuhusu bima kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Mamlaka (CSP), ikiwa ni sehemu ya juhudi za kupanua uelewa na wigo wa soko la bima nchini.

Pia, Ofisi za TIRA kanda ya kati zipo jijini Dodoma, mtaa wa Makole jengo la PSSSF House ghorofa ya 5 na kanda hii pia inahudumia mikoa ya Iringa na Manyara katika kutekeleza majukumu yake.

Ana kwa Ana

na Hadija Maulid

TIRA Kanda ya Mashariki na Mikakati Kuimarisha Sekta ya Bima

Mpendwa Msomaji wetu wa TIRA Upadates, karibu katika ukurasa huu unaokuleta maswala mbalimbali yanayojiri katika sekta ya bima ukikutanisha na wadau mbalimbali wakielezea yanayojiri katika maeneo yao ya utendaji.

Na toleo hili linakukutanisha na Meneja TIRA Kanda ya Mashariki yenye ofisi zake jijini Dar es Salaam.

Karibu!

Kwenye ukurasa wetu wa Ana kwa Ana tunakuletea mahojiano maalum kati ya Meneja Uhusiano na Mawasiliano Bi. Hadija Maulid na Meneja wa Kanda ya Mashariki Bw. Zakaria Muyengi. Karibu kwenye ukurasa huu kujua masuala mbalimbali kuhusu Kanda hii.

Kanda ya Mashariki yenye ofisi zake zilizopo Manispaa ya Ubungo: Barabara ya Sam Nujoma, Jengo la PSSSF Commercial Complex ghorofa ya Tatu, jijini Dar es Salaam inaundwa na Mikoa mitatu ambayo ni Dar es Salaam, Pwani na mkoa wa Morogoro uliopo tarkiban kilometa 200 upande wa Mashariki wa Dar es Salaam.

Mwaka 2024, Kamishna wa Bima Tanzania Dkt. Baghayo Saqware kama kiongozi Mkuu wa Mamlaka alimteua Meneja Bw. Zakaria Muyengi kuongeza kanda hiyo. Aidha, Kanda ya Mashariki ina watumishi nane (8) ambao ni mahiri na wenye ujuzi wa masuala ya bima na tawimu bima.

Watumishi hawa kwa kusaidiana na Meneja wamekuwa wakitekeleza majukumu yao ya kila siku ambayo ni pamoja na; kufanya usajili wa watoa huduma za bima, utoaji wa elimu ya bima kwa umma, kushughulikia malalamiko ya wakata bima, kufanya ukaguzi wa watoa huduma na pia kushirikiana na taasisi mbalimbali kama vile jeshi la polisi na LATRA kusimamia ukaguzi wa bima kwenye vyombo vya moto kwa mujibu wa Sheria na Taratibu.

Kanda ya Mashairiki inajitanabahisha kwa kudumisha ushirikiano wake na Taasisi mbalimbali za umma na binafsi katika kuchochea maendeleo ya sekta bima ikiwa ni pamoja na kufanya semina,warsha, mikutano na kushiriki kwenye maonesho ya kitaifa na kimataifa.

Je wananchi wanasikilizwa kwa njia gani? Mbinu mbalimbali zinatumika katika kuwahudumia wananchi ikiwemo kupokea na kusikiliza maoni, mahitaji yao na changamoto mbalimbali, mfano katika mwaka wa Fedha unaomalizikia Juni mwaka huu wa 2025, Kanda ya Mashariki imepiga hatua kubwa ya kuwasikiliza wananchi kwa kuwafuata hadi katika maeneo yao kwa lengo la kuwasikiliza na kupata maoni yao na changamoto ambazo wanakutana nazo.

Hivi karibuni Kanda imeanzisha madawati ya kupokea maoni na malalamiko kutoka kwa wananchi kupitia ofisi za wakuu wa Mikoa ya Pwani na Morogoro. TIRA kupitia kanda ya Mashariki inaamini kwamba uongezaji wa wigo huu hadi maeneo ya wananchi kutachochea na kuimarisha upatikanaji wa huduma za bima.

Meneja Muyengi ameendelea kufafanua namna wanavyopata maoni kwa njia za kukutana na wadau anasema "Angalau mara mbili kwa wiki tunakuwa na kikao na wadau wetu kupata maoni usuluhishi, kupokea na kutatua changamoto za wadau kwenye soko la bima. Mamlaka pia imeweka mfumo wa kupokea maoni au malalamiko kwa kupitia kupiga simu, kuandika barua na barua pepe (email)".

Si hivyo tu, Kanda inahakikisha haki za mteja wa bima na haki za kampuni za bima zinalindwa ili kuhakikisha maslahi ya kila upandwe yanalindwa. Kanda hii hushughulikia malalamiko kutoka kwa wateja hasa fidia kutokulipwa, kucheleweshwa au fidia isiyostahili kutoka kwa watoa huduma.

Kanda hii hutatua changamoto hii kwa vikao kwa kukutana na pande zote mbili lakini pia kwa barua za maelekezo stahiki kwa kampuni za bima. "Tunashukru ushirikiano tunaopata kutoka kwa kampuni za bima kwenye ulipaji wa madai, kwa sabau tunaamini kampuni isiyolipa madai halai ni kampuni mfu na inafanana na mcheza upatu" aliongeza Muyengi.

Hali ya usajili ikoje? Kanda ya Mashairiki inaandikisha na kutoa leseni mbalimbali kama vile leseni za madalali, mawakala, waendesha huduma za afya, wakadria hasara na magereji.

Kanda na wateja wake inanufaika na ubunifu wa mifumo ya usajili ya ORS. Kupitia ORS mambo yamerahisishwa sana ambapo mteja haitaji kutembelea ofisi zetu badala yake anaweza kupata huduma hiyo kutumia simu yake popote alipo duniani.

Je, ungependa kufahamu namna ukaguzi wa kampuni kwa ngazi ya Kanda unavyofanyika? Kuna mpango wa pamoja wa ukaguzi ambao unasimamiwa na Kurugenzi ya Ukaguzi. Kanda zinatekeleza mpango huu kwa kuchagua kampuni za kukagua kwa kila robo ya mwaka. Aidha, kuna kampuni ambazo zinaweza kukaguliwa muda wowote kutegemeana na uhitaji.

Kama Kanda wamejiandaa vipi na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya 2023? Bima ya afya kwa wote imeanza kutekelezwa na kanda ya Mashariki imeendelea na uhamasishaji kwa umma kufahamu majukumu ya TIRA na pia majukumu ya skimu za bima.

Aidha eneo la vifurushi kwa makundi mbalimbali pialimeendelea kuandaliwa na kutolewa miongozo ambayo itatoka hivi karibuni. Kwa upande wa miundo mbinu ya kiteknolojia, Kanda imeendelea kushirikiana na kitengo cha ICT kuhakikisha kwamba skimu zote za utoaji huduma ya bima ya afya zinajisajili kwa ajili ya kuwa na takwimu za pamoja.

TANZANIA INSURANCE REGULATORY AUTHORITY
TANZANIA INSURANCE
REGULATORY AUTHOR
(TIRA)
TIRA Updates 2025
PBZ BANK
BIMA
Ni Kinga,
Uhakika wa Matibabu ni Kuwa na Bima ya Afya!
TIRA Updates 2025
Uhakika wa Matibabu ni Kuwa na Bima ya Afya!
Our Vision
A World-Class Insurance Re
Our Value
Professionalism, Customer Cen

TIRA
TANZANIA INSURANCE REGULATORY AUTHORITY
TANZANIA INSURANCE
REGULATORY AUTHORIT
(TIRA)
Our Miss
develop, promote and
Our Values
World-Class Insurance Regulator

Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara

Bima ni nini?

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uMeinga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.

TIRA & 2025

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

FB, IG, X: //@tira_tz
www.tira.go.tz